

Shamte Kilalile

Natamani Kukusahau

HAKIMILIKI

Hakimiliki© 2021 Shamte Juma Kilalile

Haki zote zimehifadhiwa. Kwa malipo ya gharama husika umeruhusiwa kusoma kitabu hiki. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupakua au kusambaza bila idhini ya kimaandishi kutoka kwa Mwandishi. Hatua kali za kisheria zitachukuliwa kwa atakayekiuka.

Kitabu hiki ni kazi ya kufikirika. Majina, Wahusika, Matukio na Maneno yote vimetokana na fikra ya Mwandishi na wala havihusiani na mtu, watu, tukio au sehemu.

Shamte J. Kilalile
Kijichi, Dar Es Salaam
Tanzania

Yaliyomo

HAKIMILIKI	2
DIBAJI	4
O1.....	1
O2.....	7
O3	12
O4	17
O5	20
KAZI ZINGINE ZA SHAMTE KILALILE.....	28
KUHUSU MUANDISHI.....	29

DIBAJI

Alikuwa ni mwanamke aliyenifanya niwaache wanawake zangu wote niliokuwa nao ili nibaki na yeye tu.

Machoni mwangu alikuwa mrembo zaidi kuliko wanawake wote niliowahi kuwa nao.

Masikioni mwangu alikuwa na sauti nzuri zaidi kuliko nilizowahi kuzisikia.

Na kikubwa tulishabihiana kwenye vipaji vyetu vya kuimba mziki.

Lakini siku tulipokuja kuachana, aliondoka na kila chembe ya hisia ya kupenda tena mwanamke mwengine isipokuwa yeye.

01

Tegeta Wazo, 2021

Nilihisi ningeweza kumsahau. Lakini haikuwa rahisi kama nilivyodhani.

Ni kama jana vile, kumbe imeshapita miezi mitatu sasa. Miwili kati ya hiyo, ilikuwa miezi ya maumivu ya moyo,

Miezi ya upweke,

Miezi ya kunywa pombe sana japokuwa hazikunileweshwa katu.

Ukurasa wangu wa Instagram ulikuwa kimya. Sikuweza kuweka cover ya nyimbo yoyote niliyoifanya.

Waandishi wa habari na kurasa wa udaku kila walipotaka kufanya mahojiano na mimi niliwakwepa kama ukoma. Sikuona sababu ya kuongelea chochote kwa sababu kuu tatu; heshima ya kuwa yeye ni mama wa mtoto wangu, mustakabali wa mtoto mbeleni atakapokuja kuwa mkubwa na mapenzi ambayo bado nilikuwa nayo juu yake.

Sasa mwezi wa tatu huu, japokuwa nimeweza kuachana na pombe kabisa, maumivu ya moyo yamepungua kiasi na ukurasa wangu wa Instagram umeanza kupata uhai wa kuweka covers mbili tatu ila bado sijaweza kumsahau.

Lau kama isingekuwa mtoto niliyezaa nae, Brandina Yohana Mashauri au Bryma kama anavyojulikana na wengi mitandaoni, ningemuingiza kwenye kundi la wanadamu ambao ninawachukia zaidi duniani. Nimekuwa kama mwanajeshi mstaafu aliyesahau kutumia silaha zake, japokuwa sijui kama mwanajeshi huyo yupo ila ndio hali ninayoipitia hivi sasa.

Asubuhi hii ya Alhamisi, nikiwa nimelala kitandani nikakumbuka yakuwa usiku wa leo majira ya saa tano ninatakiwa kuwa katika kipindi cha redio cha Chumba cha Mahaba kinachofanywa na mtangazaji Jay Styles wa City fm kwa ajili ya kufanya covers ya nyimbo mbalimbali za kimapenzi.

Niligeuka na kuchukua simu yangu iliyoko kwenye kimeza kidogo pembeni ya kitanda na kuangalia saa, majira yalisoma saa tatu na dakika tano. Nikawasha data ili jumbe za mitandao ya kijamii ziingie kisha nirudisha simu kwenye meza na kuamka na kuelekea

dirishani huku nikiimba nyimbo ya *I Will Make Love To You* wa Boys II Men kama moja ya nyimbo moja wapo niliyoandaa kwa ajili ya kipindi cha Jay Styles,

*Close your eyes, make a wish
And blow out the candlelight
For tonight is just your night
We're gonna celebrate,
All through the night*

*Pour the wine, light the fire
Girl your wish is my command
I submit to your demands
I will do anything,
Girl you need only ask*

*I'll make love to you
Like you want me to
And I'll hold you tight
Baby all through the night
I'll make love to you
When you want me to
And I will not let go
Till you tell me to*

*Girl relax, let's go slow
I ain't got nowhere to go
I'm just gonna concentrate on you
Girl are you ready?
It's gonna be a long night*

*Throw your clothes on the floor
I'm gonna take my clothes off too...*

Nilipofika mstari huo nilinyamaza hasa baada ya kufika dirishani na kuona mvua kubwa ikinyesha.

This won't work, niliwaza.

Mstari huu uliyasukuma mawazo yangu mbali kidogo. Niligeuka na kukiangalia kitanda changu nilichotoka kukilalia muda si mrefu, kilikuwa kati hali ya upweke, upweke ambao si kawaida yake kuwa nacho.

Kipindi cha nyuma kabla ya kukutana na Bryma, majira kama haya ya hali ya hewa, yalikuwa majira pendwa kwangu kwani kitanda hiki cha chuma cha futi sita kwa sita kilinesa kwa mikikimikiki

yangu na wanawake tofauti tofauti niliokuwa nikiwabadilisha kila iitwayo siku.

Kuachana kwangu na Bryma kulinifanya kukosa kabisa hamu ya kutamani mwanamke mwengine yoyote yule. Mademu zangu wa zamani ambao niliamua kuwapiga chini baada ya kuanza mahusiano na Bryma, waliposikia habari za kuachana kwetu walianza kunimiminia simu mfululizo.

Wa kwanza alikuwa Jane Membe, mtoto wa Ephraim Membe aliyekuwa balozi mstaafu wa Tanzania nchini Kenya. Si tu nilikuwa nimefuta namba yake bali hata sauti yake nilikwishaisahau.

Ilikuwa zimepita siku mbili tu toka nibwagane na Bryma. Siku ile nilirudi nyumbani nikiwa nimekunywa bia nyingi ambazo kama kawaida hazikunilewesha kutokana na wingi wa mawazo.

Simu ya Jane iliingia saa sita usiku nikijianda kujirusha kitandani kutafuta usingizi.

"Morris nasikia umeachana na yule changudoa wako", sauti nyororo ya Jane ilisikika kwenye ngoma za masikio yangu.

Ana bahati sana hakumuita Bryma hivyo mbele yangu maana sijui ningemfanyaje kutokana na hasira nilizokuwa nazo. Niliamua kumbwatukia, "na wewe ni malaya gani unaenipigia muda huu wa kulala?"

Jane alicheka kwa kicheko cha kebehi, "usingizi wenyewe utakuwa nao basi au ndio kujishaua? Ungekuwa mtu wa kulala ungeshalala zamani"

"utajitambulisha au ndio nikukatie simu?", niliuliza kwa sauti ya ukali

"Mimi Jane, mpenzi wako Jane Membe. Unanikumbuka?"

"Sina mpenzi anaitwa Jane na kama ningekuwa nae sioni kama kuna haja ya kumkumbuka"

Jane alicheka tena, "wewe nawe kwa majibu ila najua ni hasira tu na zitaisha tu nikiya kwako kukufanyia vile vitu nilivyokuwa nikikufanyia"

"kwani hapo wadini kwenu wanaruhusu wendawazimu kupiga simu au umeshapona?"

"Morris!", Jane aling'aka kwa sauti ya hasira, "yaani unaniita mimi mwandawazimu kweli!?"

Roho yangu ilisuuzika kidogo kwa kujua wala nimentibua kama alivyonitubua mimi. Ila kwa uzoefu wangu na hawa wanawake niliokwisha kuwa nao kimahusiano, najua hata niwatibue vipi huwa hawanikatii tamaa. Na hii ni kwa sababu huwa nawapa vitu ambavyo ninahakikisha hata waende wapi hawanisahau.

"ila sawa wewe nijibu tu unavyotaka labda sijui unajua kwa sababu nakupenda", Jane alilalamika

"umemaliza?"

"nimerudi nchini Morris nina wiki sasa. Nimesikia umeachana na Bryma nikaona nikucheki nikahisi huwenda ukahitaji kampani"

"nafikiri utakuwa umehisi vibaya sina haja ya kampani. Usiku mwema", nikakata simu.

Mwanamke wa pili alikuwa Raya Salumu, mtoto mmoja wa kiarabu niliyemaliza nae shule moja ya sekondari kisha akatokomea nchini Marekani kwa ajili ya masomo zaidi.

Nilikutana na Raya pale Hunters Club, Oysterbay wiki mbili tu toka arejee nchini. Baada ya kumaliza burudani, usiku ule tuliumaliza nyumbani kwao mitaa ya Regent Estate, Kinondoni.

Raya aliniambia anaishi na dada yake tu kwenye nyumba hiyo na wazazi wao wanaishi Ununio na hawana kawaida ya kuja hapo isipokuwa yeye na dada yake ndio huwa wanawatembelea. Hivyo sikuwa na hofu hata kidogo ya kujiachia.

Nilikuwa na Raya kwenye mahusiano kwa miezi miwili tu na kuachana naye baada ya tukio ambalo nilihisi ningetolewa roho yangu.

Siku moja kulipopambazuka, nilimuacha Raya chumbani kwake akiwa amelala fofofo nami nikawa nazungukazunguka kwenye jumba lile. Lahaulah! nikakutana na mwanaume aliyevalia vazi la mwambao la msuli, fulana nyeupe na kidevuni alikiwa mwenye ndevu nyingi sana za rangi ya wekundu na njano.

Nikahisi atakuwa aliingia usiku sana wakati sisi tukiwa tumelala. Maadamu Raya aliniambia anaishi na dada yake na wala

yeye na dada yake hawakuona tabu kuniambia kuwa kuna aina hii ya wanaume huwa wanakujakuja hapa nyumbani kwao nikajua hawa washenzi wameniingiza choo cha kike na sikujua walikuwa wana nia gani na roho yangu.

Sikutaka kujua yeye ni nani wala kuulizwa mimi ni nani na nimefata nini pale, niligeuka na kukimbia kwa kasi ya ajabu na wala sikumbuki niliwazaje kuruka ule ukuta mrefu maana nilijua nikimbilia getini kwa mlinzi haitakuwa salama kwangu.

Sikutaka tena kuwasiliana na Raya japokuwa aliniganda kama luba. Ilibidi nimblock kila sehemu kuepuka usumbufu zaidi. Kupitia namba mpya, simu yake iliingia asubuhi na mapema nikijianda kwenda kufanya mazoezi.

"Morris, Morris, Morris, I never thought there will be any girl to dump you, yet, Bryma shows up to prove me wrong"

Nilimuahidi Bryma, hata kama nitahojiwa na vyombo vya habari, katu sitakuja kusema chanzo cha kuachana kwetu japokuwa yeye aliahidi kunichafua. Nilijua kama nitakuja kukisema hiki chanzo bila shaka ningeweza kutengeneza kitu kibaya sana mbele ya safari baina ya mwanangu na mama yake na hata mimi mwenyewe.

Hata shetani kuna wakati anamuogopa Mungu. Nami licha ya ushenzi wangu wote wa kupenda wanawake katu sijafikia ushenzi na ujasiri wa kufanya kitu ambacho Bryma alitaka tufanye.

Ni kawaida yangu nikiwa faragha na mwanamke, kufanya na kujaribu namna na njia mbalimbali za kunogesha tendo. Na kwa Bryma haikuwa tofauti mpaka siku moja alipotaka tufanye utundu wa kumuendea kinyume na maumbile. Nilimweleza siwezi na haitawezekana. Hali ilipozidi ya kunilazimisha na kunitaka tufanye kile kitendo, ilibidi tuachane.

Sasa nitaanza kusema vipi hili mitandaoni na kwa maandishi wa habari halafu siku moja mwanangu akikua mkubwa aje kuona baba mtu nikimsema vibaya mama yake kwa uchafu huu?

Mwanangu atanionaje?

Atamwonaje mama yake?

Na nani ataniamini?

Na kwa faida gani?

Hivyo wa busara zangu tu niliamua kunyamaza hata kama wanawake kama Raya wataona nimebwagwa wacha iwe hivyo.

Hivyo nilimjibu, *"what does it matter to you if I'm dumped?"*

"Nothing. Though you block me everywhere I thought I should pay back at least by laughing at your face", kisha alicheka sana kwa dharau.

Niling'ata meno kwa hasira.

Alipomaliza kicheko chake, nilimuuliza.

"Satisfied?"

"Satisfied", alikariri neno langu kwa kugeza sauti yangu ya besi.

"Talking like a tough man uuh? Well, I think I will look for this Bryma. She needs little present from me", kisha alicheka tena

Nikaona kwa dharau hizi sasa inatosha, nilikata simu kwa hasira na kurudi zangu chumbani.

Safari ya mazoezi iliishia hapo.

02

Kisha zilifatia simu za wanawake zangu wengine; Suzan, Jessica, Florence, Riyama, Loveness, Joyce, Witness, Lightness, Hamisa, Asia, Dayna na wengine hata siwakumbuki.

Si hawa wala wengine niliokutana nao barabarani waliweza kuibua hisia zangu tena. Ni kana kwamba Bryma aliondoka na uwanaume wangu wote na sikujua hali hii itaisha lini.

Taratibu nilielekea bafuni nikiwa naimba wimbo wa *What is Love* wa V Bozeman,

*I would tell you that I love you tonight
But I know that I've got time on my side
Where you goin'? Why you leavin' so soon?
Is there somewhere else that's better for you?*

*What is love if you're not here with me?
What is love if it's not guaranteed?
What is love if it just ups and leaves?*

*What is love if you're not here no more?
What is love if you're not really sure?
What is love?
What is love?*

*Told myself I wouldn't cry when you're gone
But I know it's easier said than done
Look at me, look at me, choked up now
Try to tell you but it won't come out*

Nikanyamaza baada ya kusikia kwenye bati la nyumba kama mvua inafifia. Niligeuka kuchugulia dirishani, ni kweli.

Bora, nilijisemea moyoni.

Nilitabasamu maana mvua kwangu tena haikuwa na maana. Niligeuka tena na kuendelea na safari ya bafuni huku nyimbo ya V Bozman ukirudi mdomoni,

*I can't live without you
I can't live with you
What goes around will come right back around
You won't know 'til it hits you
We were supposed to be (an empire)
We were supposed to be (an empire)
We were supposed to be an empire*

*What is love if you're not here with me?
What is love if it's not guaranteed?
What is love if it just ups and leaves?*

*What is love?
What is love if you're not really sure?
What is love if it just ups?*

Baada ya dakika kumi na tano nilirejea chumbani nikiwa nimejifunga taalo kiunoni na kwenda kuinyanyua simu yangu na kuangalia *notifications* za Instagram.

Macho yangu yalikutana na *notification* ya Nick Mastory, moja ya akaunti za habari na udaku mtandaoni. Niliibonyeza.

Sikuweza kuamini masikio na macho yangu kwa kile nilichokuwa nakiona kwenye kioo cha simu yangu. Japokuwa aliahidi kunichafua ila sikutegemea kama ingekuwa kwa kiwango hichi.

Najua kama mwanadamu nina mapungufu yangu lakini si kwa kiasi hiki ambacho Bryma, mwanamke huyu ambaye nilimpenda kwa moyo wangu wote alikuwa akiyasema mbele ya mwandishi wa habari.

Niliwaza siku itakuwaje kama mwanangu akiya kuona mahojiano haya na kauli hizi za mama yake juu yangu. Roho iliniuma sana.

Bryma alikuwa ni msichana mwenye ngozi nyeusi yenye kunga'aa. Kwenye mahojiano haya alikuwa amevaa gauni jekundu la umbile la *mermaid* lilomkamata vizuri mwili wake na kuchora umbo lake zuri. Chuchu na hipsi zake zilichomoza kana kwamba zilikuwa zikidai uhuru wake ambao gauni ulikuwa ukizinyima. Juu ya macho yake legevu kulikuwa na nyusi ambazo zilipakwa wanja mwembamba mithili ya mbalamwezi. Uso wake wa mviringo uling'aa kutokana

makeup aliyopaka huku midomo yake mipana ikiwa imekolea rangi nyekundu kumechisha na rangi ya gauni.

Alisimama juu ya kapeti ya rangi ya nyekundu huku nyuma yake kukiwa na bango lenye nembo za kampuni mbalimbali kuashiria alikuwa kwenye mfano wa tafrija au tamasha fulani. Nikahisi mahali pale panaweza kuwa Mlimani City au JNICC. Pembeni yake alisimama mwandishi wa kiume, *mic* mkononi akiwa amelelekeza mdomoni mwake.

"mwanaume malaya sana yule", alisema Bryma

"kwanini unasema hivyo?", aliuliza mwandishi kwa kuirudisha *mic* mdomoni mwake kisha kumrudishia tena Bryma

"mimi ni mtu mzima sina haja ya kuyasema yote hapa, we jua hivyo tu"

"kwa hiyo ndio mmeachana?"

"kama unavyoniona mtoto wa kike, wewe huoni hata rangi yangu inaanza kurudi rudi", aliongea Bryma huku akizungusha zungusha mashavu yake kumuonyesha mwandishi, "maana nilifubaa haswaa"

"kwa hiyo hauna mpango wa kurudiana tena?", aliuliza mwandishi

"kwa kipi!? Nimesahau kitu gani kwake!?"

"kwa sababu si mara ya kwanza wewe na yeye kuachana"

"babu wee achana na zilipendwa hizo. Sasa hivi Bryma mimi sio wa kuyarudia yale matapishi"

"unasema!?"

"ndiyo hivyo babu. Yale matapishi tu"

"Usiseme hivyo Bryma jua ni mzazi mwenzako yule"

"uzazi huo kwio! Mwanaume hata kuhudumia mwanamke wake hajui, wa kazi gani mie" Bryma alicheka kwa dharua huku akibenuabenua midomo yake.

"acha bwana, unajua wambea wanakusikiliza Bryma"

"tena wanisikie vizuri hasa wale wanaume suruali kama huyo mwenzao", alizungusha zungusha macho yake kwa dharau, "Unajua

mapenzi nyoko eenh! Mapenzi nyoko sana yaani sijui hata ilikuwaje nilimuacha yule mwanaume wangu wa Masaki na kukubali kuishi na mwanaume hata hajui kukua ni nini"

"Una maana gani unaposema hajui kukua?"

"aah bwana weee, mtu hajui kuhudumia mwanamke wake. Anachojua yeye ni kukaa na washikaji zake kupiga stori, kuimba imba, kunipiga na kuni... pale nye... zikimshika" nilisikia sauti za ving'ola kuashiria hayo ni maneno ambayo kimaadili ya utangazaji hayakutakiwa kusikika.

Muandishi wa habari alicheka kisha, "yaani ulivyokuwa unapendeza kipindi cha mahusiano yenu unataka kusema alikuwa hakuhudumii?"

Bryma alicheka kwa dharau kisha, "usinichekeshe mie"

"Kwa hiyo alikuwa anakuhudumia nani kipindi chote kile?"

"Usiulize mwanamke anajihudumiaje pindi mwanaume wake akishindwa kuhudumia", Bryma aliongea huku akijitingisha kwa madoido

"Ulikuwa una danga?"

"sijui", alibenua midomo huku akiangalia pembeni

Alicheka tena mwandishi kisha aliita jina lake kwa kulivuta, "Brymaaaaa"

"ndiyo mimi. Umemaliza maswali yako maana nataka nirudi nyumbani nikampuzike maana kuna Mwanaume kamili huko ananisuburi"

Sikuweza kuendelea kuangalia zaidi mahojiano yale. Bila shaka Bryma alikusudia kunitibua haswa ili tu apate sababu zaidi ya kunichafua hasa nitakapoamua kuchukua na kumtenga katika kutoa huduma kwa mtoto.

Niliikumbuka siku ile ya kwanza nilipokutana na Bryma kwenye sherehe ya rafiki yangu Baraka na mkewe Joan katika kutimiza miaka mitano ya ndoa yao.

Nyimbo ya kwanza aliyoimba Bryma jukwaani ilikuwa ni *Bones* ya Maren Morris. Japokuwa alikuwa akiimba kwa ajili Baraka na Joan ila moyo na nafsi yangu vilihisi wimbo ule ulikuwa maalumu kwa ajili yetu.

What happen to us? What happen to our bones? Nilijiuliza moyoni.

Niliweka simu mezani kisha nikalaza kichwa changu kwenye mto wa kitanda nikaanza kukuimba wimbo ule wa Bones,

*We're in the homestretch of the high times
We took a hard left
But we're alright
Yeah, life sure can try to put love through it, but
We built this right, so nothing's ever gonna move it*

*When the bones are good, the rest don't matter
Yeah, the paint could peel, the glass could shatter
Let it break 'cause you and I remain the same
When there ain't a crack in the foundation
Baby, I know any storm we're facing
Will blow right over while we stay put
The house don't fall when the bones are good*

*Call it dumb luck, but baby, you and I
Can't even mess it up although we both try
No, it don't always go the way we planned it
But the wolves came and went and we're still standing*

*When the bones are good, the rest don't matter
Yeah, the paint could peel, the glass could shatter
Let it break 'cause you and I remain the same
When there ain't a crack in the foundation
Baby, I know any storm we're facing
Will blow right over while we stay put
The house don't fall when my bones are good
When the bones are good*

Nyimbo hii ilinisafirisha mwaka mmoja nyuma na kunipeleka mpaka hoteli ya Sapphire ambapo ndio ilikuwa mwanzo wa safari ya kukutana na Bryma.

03

Ilikuwa ni miongoni mwa siku za katikati ya wiki mimi na rafiki yangu Baraka Kalinga tulikuwa tukipata chakula cha mchana Kariakoo katika hoteli moja iitwayo Sapphire iliyopo mtaa wa Somali.

Baada ya kuongea mambo mbalimbali hatimaye Baraka alinishirikisha kwenye jambo lake ambalo alihitaji msaada wangu.

"Morris naomba msaada wako", Baraka aliniambia

"kuna nini?"

"unajua ni miaka mitano sasa toka mimi na Joan tufunge ndoa. Tulipanga kufanya katafrija kadogo ka kuadhimisha kipindi chote hiki cha ndoa yetu"

Nilicheka kwanza kisha niliuliza kwa utani, "miaka mitano unataka kufanya *anniversary*? Na hao wenye miaka ishirini wasemaje?"

"watasema wanayotaka kusema ila mimi na Joan tunasema na tumeamua kufanya hii tafrija"

Nilicheka tena, mara hii kwa nguvu zaidi.

Baraka aliendelea kuongea, "wewe unajua zama zetu hizi kukaa mwaka tu kwenye ndoa ni shughuli sasa huoni sisi tumejitahidi kidogo kuvumiliana ndani ya miaka hiyo mitano"

"ni kweli"

"ni kama jana vile tulipomuona Joan"

Nilitingisha kichwa kuafiki, "*funny how people meet*", niliongea huku nikizungushazungusha macho ndani ya ile hoteli

"tena ilikuwa kwenye hoteli hii hii", Baraka alicheka sana kisha aliongeza, "*She was quite a doll that day Morris, won't you agree?*"

Baraka aliongea kwa tabasamu huku macho yake yakionyesha ni mwanaume aliyezama kwenye mapenzi haswa.

Nilimtazama na kutoa tabasamu hafifu huku kichwani nikiwaza kama na mimi ningekuja kupata muonekano kama huo.

Miaka mitano iliyopita, msichana mmoja umri baina ya miaka ishirini na tano na thelathini, sio katika daraja la wanawake ambao wangeweza kunivutia, alikaa katika moja ya kona ya Hoteli ya Sapphire huku uso wake ukiwa na wasiwasi na macho yake yalikuwa yakitazama saa yake ya mkononi na simu iliyoko mezani kila mara.

Alivalia kigauni cha rangi nyeupe ambacho kwa uoni wa macho yangu chini ya meza aliyokuwepo kiliishia kwenye magoti na kufanya miguu yake miembamba kuonekana. Alikuwa mweusi wa rangi na machoni alivalia miwani yamkini itakuwa ni kwa ajili ya macho. Alikuwa ni aina ya wale wasichana wenye maumbo fulani madogo.

Mezani kwake kulikuwa na simu pamoja *glass* ya juice iliyokuwa nusu.

Meza ya mimi na Baraka ilikuwa mkabala na meza aliyokaa msichana huyu. Mezani kukiwa na *glass* ya juice upande wa Baraka na bia upande wangu.

"Unadhani atakuwa anamsubiria mtu?", aliuliza Baraka huku akimkodolea binti yule kwa macho ya uwizi uwizi.

"Nadhani bwana wake atakuwa amempotezea"

"Unahisi hivyo!?"

"Sio kwa muonekano ule", nilimuangalia binti yule ambaye sasa alikuwa ameweka simu masikioni kisha aliitoa na kuiweka tena mithili ya mtu aliyekuwa anapiga simu mara kwa mara, "mwanamke akiwa kwenye hali ile bila shaka ni *boyfriend trouble*", niliongezea

"Ila sio poa kabisa kumfanyia hivyo mwanamke ni bora kumuambia kuliko kumuacha mpaka kufika eneo la miadi"

Nilicheka kisha sikusema kitu.

Baraka aliniangalia kwa butwaa, "una tatizo gani!? Mbona unacheke?"

"Hivi unajua wanawake wanawapotezea wanaume zaidi kuliko wanaume wanavyowapotezea wanawake?"

"Utafiti huo kafanya nani?"

"Hebu niambie ni mara ngapi wanaume wanatuma hela ya nauli kwa wanawake ili wafike sehemu waliyokubaliana mwisho wa siku hakuna kitu"

"Kwa hiyo una *support*?"

"Kwa demu kama yule ...", nilimuangalia tena yule msichana ambaye sasa alikuwa ameinama na kuitoa miwani yake na kufuta macho yake, "nahisi analia", nilirudisha macho kwa Baraka, "mfate huwenda akahitaji kampani yako bro"

Kana kwamba Baraka hakusikia kauli yangu ya mwisho alirudia maneno yangu huku akiwa amenikazia macho, "Umesema kwa binti kama yule, umemaanisha nini?"

Nilitaka kusema *hata ningekuwa mimi ningempotezea* ila kwa jicho lile nilihisi Baraka atakuwa amevutiwa na yule binti hivyo nilifikiria cha kusema.

Nilikunywa fundu moja la bia kisha niliishusha glass kwenye meza huku nikiiangalia kwa muda kisha nikasema, "unajua muda mwengine nashindwa kutofautisha kipi kitamu kati ya bia na sex. Huyu aliyebuni bia nahisi alikuwa mkali sana wa mademu. Wewe unaonaje Baraka?", niliongea huku macho bado yapo kwenye glass ile ya bia

"Hivi kwanini lakini nakosa ushirikiano wako katika hili?"

Nilinyanyua macho yangu kumuangalia Baraka. Nilikutana ana kwa ana na jicho lake kali,

"Relax", nilisema huku nikitabasamu, "nimeuliza tu kaka"

"Yaani mimi naongelea vitu vya maana wewe unaongelea bia"

"Vya maana ukimaanisha yule?", niligeuka kumuangalia tena yule binti ambaye bado uso wake ulikuwa hauna utulivu huku glass yake ya juice ikiwa bado iko nusu kisha nilirudisha macho kwa Baraka.

"Unajua hupaswi kuwaongelea hivyo wanawake kama vile sijui kinyaa au kitu gani sijui"

"Kwani wapi umesikia nimemuongelea vibaya yule dada wa watu?"

"Si hayo macho yako"

"Macho yangu yanaamanisha yule siyo aina ya wanawake ambao nawafukuzia. Robo saa nzima unaniuliza maswali kuhusu yeye ambayo sina haja nayo wala sijui majibu yake. Nikikuuliza kama una mtaka unakwepa kunijibu *direct*"

"Kwa hiyo una maanisha nini?"

"Unataka ushirikiano wangu nijibu swali langu tofauti na hapo nitakukatisha tamaa tu kwa majibu yangu huku sijui nia yako. Kwa hiyo narudia tena, unamtaka?"

Baraka alinyamaza kwa muda huku akiniangalia kwa makini kisha aliegemea kiti, "unajua muda mwengine nashindwa kujua wewe ni mtu wa aina gani", alinyanyua glass yake ya juice na kunywa funda moja na kuirudisha mezani, *"Sometimes you are son of the bitch and sometimes..., well... I don't know"*

Nilitabasamu, "hata shetani muda mwengine hugeuka na kuwa malaika"

Aligeuka tena kumuangalia tena yule msichana, ambaye mara hii alikuwa akirudisha kiti nyuma ishara ya kutaka kuondoka,

"Yeah I think I want her", Baraka aliongea huku macho bado yako upande ule aliko yule msichana, *"and am going to talk to her"*

Kwa urafiki wetu wa muda mrefu sijawahi kuona Baraka akimuangalia mwanamke yoyote yule kwa namna ambayo alikuwa akimuangalia huyu msichana. Hapo ndipo nilijua jamaa yangu atakuwa amekamatika. Ilibidi nimpe maneno ya ushirikiano.

"Go tiger before she disappears for good"

Baraka alinyanyuka kwa haraka na kupiga hatua ndefu ndefu kuelekea meza ya msichana yule ambaye mara hii alikuwa amesimama huku akiweka simu yake kwenye kijipochi kidogo kwa ajili ya kuondoka. Alitulia kwa muda huku akiwa amejiinamia kuiangalia meza yake.

Baraka alipofika, msichana yule alinyanyua macho yake na kumuangalia.

Nikaona midomo ya Baraka ikifunguka.

Yule msichana alinyanyua mkono wake juu ikiwa ni ishara ya kumuambia Baraka kunyamaza au kutokuwa tayari kuongea ila niliona midomo ya Baraka ikiendelea kufanya kazi yake.

Yule msichana alitulia kimya akimsikiliza na kumuangalia Baraka kwa takribani dakika tano hatimaye niliona akitabasamu na kuangalia pembeni kisha alirudisha macho tena kwa Baraka. Hapa nilijua mzee mwenzangu ameshaula.

Taratibu msichana yule alivuta kiti na kukaa tena kisha Baraka naye akakaa kwenye kiti kingine kinachotizamana na kiti alichokalia yule msichana.

Kilichoendelea imebaki ni stori kwani hii ndio siku Baraka na Joan walikutana.

Mwezi moja baadae walifunga ndoa.

Tukirudi hotelini tena, maongezi yangu na Baraka yaliendelea,

"Najua uamini kuhusu *love at first sight* Morris lakini..."

"hapana na haitakuja kutokea. *I'm too young to fall in love at first sight but old enough to be attracted by them*",
nilimkatisha huku nikimkonyeza na kutabasamu

"Hivi utakuwa lini?"

"Siku nikikutana na mwanamke ambaye nitampenda sio kumtamani.
Tofauti na hivyo niache niwapelekee moto tu. *They are too many to ignore*"

Baraka alicheka sana na kunyanyua mikono juu ishara ya kunipa saluti.

"Bro, hebu angalia wanawake waliokuwepo humu hotelini",
niliongea huku nikizungusha zungusha macho kwenye hoteli ile iliyosheni watu wengi wanaume, wanawake na Watoto.

"Zaidi ya asilimia sabini ya mademu wote humu bado wabichi,
dizani miaka ishirini mpaka thelathini, hapo yani, na wote wakali"

Baraka alizungusha naye macho kuwangaalia wale wanawake mule ndani kisha alirudisha macho kwangu "Morris ndugu yangu kila siku wanazaliwa mademu wapya na wakali, utawamaliza lini?", aliongea kwa kusikitika

Nilianza kuimba wimbo *Pombe Sigara* wa Nviir The Storyteller,

*Pombe sigara
Naweza wacha bila kung'ang'ana,
Lakini, hawa wasichana, vile nawapenda
Ni kama laana*

*Naskia walevi huota na beer
Lakini kuna siri nitawaibia leo
See I'm not addicted to alcohol
I'm not a victim, not at all
Yalimpata Samson, yakampata Solomon*

*Situation hugeuka tricky
Kila shimo napanda miti
Contribution kwa team mafisi, Karura
Eeh, hii situation hugeuka tricky
Kwa hivyo...
Msiniweke kamba kwa shingo*

Nilipofikia mstari huo, nikasema, "Imagine, Samson ameshidwa, Solomon ameshindwa na Nviir maji kooni, anajua kuwa kuacha wanawake ni ngumu kuliko kuacha pombe na sigara, wewe ni nani kuniambia niwaache?"

Baraka alicheka, "well, ni Maisha yako sasa turudi kwenye suala langu hili la sherehe niliyokuambia"

Nilitingisha kichwa, "naam, unataka nifanye nini?"

"Nataka utuburudishe. Sikuona haja ya kuita mtu mwengine wakati wewe upo na uko vizuri kwenye kuimba. Nimekuchagua wewe na msichana mmoja nilimuona Instagram akiimbaimba covers kama wewe. Yuko vizuri nae"

"Yukoje?", niliuliza kwa hamasa

Baraka alisikitika huku akinyanyuka toka kwenye kiti ishara ya kuondoka.

"Come ooon!", niliongea huku nikirusa mikono juu, "huwezi tu kuondoka kahasara hivyo tena katikati ya maongezi"

"Eti eenh?", Baraka aliinama kuniangalia huku mikono yake ikiwa ameiweka mezani,

"Yeah"

"Basi subiri"

Baraka alimuita muhudumu mmoja wa kike kwa ajili ya kufanya malipo.

"Hata jina basi nitajie", nilimsihi Baraka

"Utamuuliza mwenyewe"

Muhudumu alifika na kumpa elfu kumi, "kata mbili dada"

"Sawa, naomba nisubiri tafadhali nikuletee chenji", alijibu yule muhudumu na kuondoka kwa mwendo wa kasi.

Akiwa bado wima, Baraka alisema, "sherehe ni jumamosi hii bro, jiandae"

"Hakuna namna ya kutukutanisha nae? Kama anaimba covers itapendeza nikifanya nae nyimbo moja ya *duo* maalumu kwako na Joan"

Baraka alicheka, "najua janja yako Morris huwezi kunipata"

"Najaribu kutoa ushauri tu ili sherehe yako ibambe. Huwezi kuliona hilo?"

"*I'm fine* kila mmoja akiimba peke yake, imeisha hiyo"

Muhudumu alirudi na cheji na kumkabidhi Baraka

"Karibuni tena", muhudumu aliongea na kutuangualia mimi na Baraka.

Kwa pamoja tuliitikia kwa vichwa vyetu.

Muhudumu akaondoka zake.

Bila kuongea zaidi, Baraka alianza kutembea kuelekea mlango wa kutokea wa Hoteli.

Nilimuangualia kisha nikacheka.

Nami nilinyanyuka na kumfata.

Jumamosi, majira ya saa tano usiku nilikuwa ndani ya ukumbi wa Savannah uliopo Quality Centre nikitoa burudani kwa kuimba covers za nyimbo mbalimbali kwenye ya sherehe ya kutimiza miaka mitano ya ndoa ya Baraka na Joan.

Mabibi kwa Mabwana waalikwa ambao ni marafiki wa wapenzi hawa walifurika kuja kuungana nao kusherehekea kwa pamoja.

Mimi nilikuwa kwenye jukwaa mbele ya wageni waalikwa nikiwa nimesimama, mic mkononi, nikimaliza kuimba beti mbili za mwisho za nyimbo iitwayo *You are the Reason* iliyoimbwa na Calum Scott na Leona Lewis.

*I don't wanna hide no more
I don't wanna cry no more
Come back I need you to hold me (You are the reason)
Be a little closer now
Just a little closer now
Come a little closer
I need you to hold me tonight

I'd climb every mountain
And swim every ocean
Just to be with you
And fix what I've broken
'Cause I need you to see
That you are the reason*

Wageni waalikwa walinyanyuka na kunipigia makofi.

"Ahsanteni sana, *thank you, thank you very much*", niliongea huku nikitabasamu na kuwashukuru kwa kuinama.

MC alitembea na kuja niliposimama huku mkononi akiwa na mic, "ahsante sana Morris kwa burudani, makofi kwake tena"

Wageni walipiga tena makofi

"Morris anapatikana Instagram kwa jina la movoice" MC alinifanyia promo kwa wageni waalikwa, "Ukimhitaji aje kuburudisha wageni wako kwenye sherehe yako basi unaweza kumpata hapo." Aliniangalia, "ahsante sana kwa burudani"

Nilitingisha kichwa ishara ya kuitikia.

"Unaweza kurudi kwenye meza yako kukaa", alisema MC akiniashiria kushuka chini ya jukwaa.

Nilishuka na kutembea moja kwa moja nyuma ya ukumbi kulikokuwa na meza moja tupu kwa ajili ya kupumzika kidogo kabla sijarudi kwenye meza yangu niliyopangiwa kukaa awali.

Nyuma yangu MC alisema, "mabibi na mabwana tuendeleo kula na kunywa huku DJ f2k akiendelea kutupa burudani kabla sijamualika mburudishaji mwengine usiku huu. Maana leo ni siku ya burudani kwenda mbele. DJ tupe vitu"

Nyimbo ya *Wivu* wa Aslay na Maua Sama ulisikika huku baadhi ya watu wakinyanyuka kulisakata rumba.

Kichwani niliwaza bila shaka MC alipotaja kuhusu mburudishaji anayefata baada yangu alikuwa akimaanisha yule msichana aliyealikwa na Baraka kuja kutumbuiza. Na mbaya zaidi mpaka sasa sijapata wasaa wa kumuona.

Nyuma ya ukumbi, kwenye meza kulikuwa na viti vitatu, nilikaa kwenye kiti kimojawapo kilichonipa wasaa wa kuangalia wageni walioko mbele yangu kwa uzuri.

Kama X ray, macho yangu yalianza kuangaza taratibu wageni wa jinsia ya kike tu huku kihoro na hamu ya kuweza walau kuotea kati ya wale ni nani anaweza kuwa yule msichana ikinishika kooni.

Jitihada zangu hazikufua dafu. Hatimaye niliona hakuna jinsi zaidi ya kusubiri akipanda jukwaani. Nilitoa simu yangu na kuinamia na kuanza kuperuzi mitandaoni.

Kwa takribani dakika ishirini nilikuwa nimezama kwenye simu yangu kiasi cha kutojua kama kuna mtu alikuja na kukaa karibu yangu kwenye moja ya viti vya ile meza niliyokuwepo.

"geez, that voice of yours can make a girl jump to bed with you",

Ilikuwa ni sauti ya kike moja nzuri sana kuisikia masikioni.

Hii haikuwa mara ya kwanza kwa watoto wa kike kusifia sauti yangu. Nimejaaliwa kuwa na sauti fulani ya kuchombeza. Sauti ambayo haikeli kuisikiliza kwenye redio hasa kwenye vile vipindi vya kimahaba vya usiku ambavyo napenda sana kama siku moja ni je kuvifanya. Na ndio sababu Instagram nilijiita moveoice.

Nilishtuka kidogo na kuangalia upande ule ambao sauti ile nzuri ilitoka na macho yangu yalikutana na msichana ambaye sikuweza kumfananisha na msichana yoyote niliyewahi kuwatia mikononi mwangu.

Yule mrembo alitabasamu kisha alisema, "samahani nimekushtua?"

Uzuri wa sura yake ukichanganya lile tabasamu lililotengeneza vijishimo mashavuni mwake, weupe wa meno yake na uzuri wa macho yake laini ulifanya moyo wangu kuruka.

Kwa dakika kadhaa niliduwa kumuangalia mrembo yule bila kusema chochote.

Aliniangalia tena mara hii kwa wasiwasi na uoga kidogo, *"I'm sorry, maybe I should go"*

"No ...", fahamu zilirudi na kuwahi kumshika mkono wake asinyanyuke, *"tafadhari usiondoke"*, niliongea kwa sauti kama ya mtu aliyeishiwa nguvu huku macho yangu hayakubanduka usoni mwake.

"Umenitisha kwa ulivyoniangalia. Nikaogopa haki yani", aliongea huku bado uso wake ukiwa nusu tabasamu, nusu wasiwasi.

Kichwa changu kilianza kupiga mahesabu ya haraka juu ya nini cha kufanya kati ya huyu mrembo aliyeko mbele yangu hivi sasa na yule mburudishaji mwenza ambaye kitambo hapo nyuma nafsi, roho na moyo wangu vilikuwa na shauku ya kumuona.

Maamuzi yangu ya mwisho yalikuwa ni kuendana na msemu usemao, *'ndege mmoja aliyeko mkononi ana thamani zaidi kuliko mia waliopo mtini'*.

Kikawaida, nimejiwekea kanuni moja muhimu sana nayo ni kumpa kila mwanamke kipaumbele chake kwa kadri alivyo na wasaa. Hivyo niliamua kama yule msichana niliyekuwa nikimsubiri atakuwa naye mkali, atakuwa kipaumbele namba mbili na suala lake

nitalishughulika wakati mwengine. Ila kwa sasa, kipaumbele namba moja na wasaa unaruhusu kwa huyu bibiye machoni mwangu.

Kwa sauti ya chini na ya kunisikia yeye tu, nilimuinamia na kuongea, "nilipokuona nilihisi nimekufa na kuona malaika peponi ila ghafla nilipoona *these creepy people...*", niligeuka kuwaangalia wageni waalikwa kisha nikarudisha macho yangu kwake, "nikajua bado niko duniani"

Yule mrembo alicheka kicheko cha nguvu kiasi cha kusikika kwa baadhi ya wageni hasa wale waliokuwa karibu yetu. Baadhi yao waligeuka na kututizama. Yule msichana aliweka mkono wake mdomoni haraka kujiziba asicheke zaidi.

Mkono wake ulikuwa na vidole virefu ambavyo ni aina fulani ya vidole vinavyonivutia kwa mtoto wa kike. Vidole virefu vina kazi yake aisee asikuambie mtu. Nilivuta pumzi ndogo.

"Ona watu walivyoniangalia. Umenifanya nimecheka kwa nguvu", hatimaye aliongea baada ya kicheko kumuisha.

"Sikuweza kujizuia kukuambia kuhusu uzuri wako"

Alitabasamu, "*you certainly know how to make a girl blush*"

Nilitabasamu, "najaribu tu, ila naomba uniwie radhi nilikuogopesha hapo awali kwa uangaliaji wangu"

"*it's okay*"

"Pale mwanzo ulisema nini kuhusu sauti yangu?"

Alicheka, "*first you make me blush and now you want to embarrass me*"

"Ila hasha, ni kwamba sikusikia tu na huwa napenda kusikia nini watu wanacomment kuhusu sauti yangu hususani mabinti"

"Woow! woow! inaonesha unapata *comments* nyingi sana kwa mabinti eenh?"

"Ni kweli ila sio kwa wale wenye uzuri kama wako"

Alicheka tena.

Vile vijishimo vyake mashavuni havikuacha kuniharibu akili yangu kila mara akicheka au kutabasamu.

Nilijikaza na kuuliza tena, "Niambie basi ulisema nini au nipotezee tu?"

"Nilisema sauti yako inaweza kumfanya mwanamke atake kulala na wewe"

"Oooh" kisha nilitulia kidogo halafu nikasema, "*will you?*"

"noooooooooo way! Besides nimeshasikia sauti nyingi nzuri sana kuliko yako", alicheka

"Oouch! *That's hurt*"

Alicheka tena, "natania bwana lakini kiukweli una sauti fulani hivi ya kiumeume *and kind of sexy though* na ukichanganya na nyimbo za kimahaba kama hii uliyotoka kuimba jukwaani ..." alitabasamu, "mmh siwezi sema zaidi"

MC aliongea kwa sauti, "jamani wanajua hawajui?"

Umati ulilipuka, "wanajuaaaaaaaaa!"

Kipindi chote nilichokuwa nikiongea na mrembo huyu kana kwamba masikio yangu yalikuwa yameziba kusikia chochote kinachoendelea ukumbini mule. Sauti ya MC ndio ilinishitua na kunijulisha bado niko ukumbini.

Niliangalia mbele na kuona Baraka na Joan wakicheza nyimbo ya taratibu huku wakiwa wamekumbatiana. Niliposikiliza kwa makini nilijua ni nyimbo ya *Always Remember Us This Way* ya Lady Gaga kutoka katika filamu ya *Star is Born*.

"*Damn! I love that song and the movie*", nilisema huku bado macho yakiwaangalia Baraka na Joan. Taratibu nilifumba macho kwa hisia na kutikisa kichwa kuendana na mdundo wa nyimbo ile na kuanza kuimba,

*So when I'm all choked up
But I can't find the words
Every time we say goodbye
Baby, it hurts
When the sun goes down*

*And the band won't play
I'll always remember us this way*

Kufikia hapa, yule msichana alidakia na kuanza kuimba na yeye,

*Lovers in the night
Poets tryin' to write
We don't know how to rhyme
But, damn, we try*

Ilikuwa ni sauti nzuri ambayo ilinifanya nifungue macho yangu na kumuangalia.

Alinyamaza na kwa muda tuliangaliana, uso wake haukukauka kwa tabasamu.

Nilimalizia mistari ya beti hii aliyoianza kuiimba huku bado tukiangaliana,

*But all I really know
You're where I wanna go
The part of me that's you will never die*

Kwa tabasamu pana, "damn! you and your voice", alisema

Nilicheka kisha kwa pamoja tuliimba kibwagizo,

*So when I'm all choked up
And I can't find the words
Every time we say goodbye
Baby, it hurts
When the sun goes down
And the band won't play
I'll always remember us this way*

"Kumbe unaweza kuimba!?", niliuliza kwa mshangao na hamasa

"Hapana najaribu sijafikia viwango vyako", alicheka

"Noo! You're goooooood, really good. You're beautiful, you've good voice and you can sing too ...", maneno yalinitoka mtoto wa kiume na mengine nikashindwa kumalizia

Unajua ile hali au hisia ambazo unaweza kuzipata pindi unapokutana na mtu ambaye vitu vingi mnafana, eenh? Basi siku hii kwa mara ya kwanza maishani mwangu ndio nilipata kuhisi hali hii. Kwa dakika chache niliona nimekutana na mwanamke wangu wa Maisha na hata ikibidi kuacha wanawake wote ili niwe na huyu mrembo nitakuwa tayari.

Niliwaza huwenda hizi ndio aina ya hisia alizopata Baraka siku ile alipomuona Joan pale hotelini kwa mara ya kwanza.

"Coming from you, thank you", aliongea msichana yule kwa bashasha

"Unaonaje tukafanya *duo* mimi na wewe?"

Kabla hajajibu nilisikia MC akisema, "sasa mabibi na mabwana napenda kumleta kwenu mwanadada ambaye atakuja kutuburidisha. Bryma tafadhali njoo mbele, tumkarabishe na makofi tafadhali"

Makofi yalianza kusikika

"I guess I'm needed", alinyanyuka na kusimama

"Wait ...", mapigo yangu ya moyo yalianza kunienda kasi.

Sikuweza kuamini kama nimepata ndege wa mkononi na wa mtini kwa pamoja. Kumbe msichana niliyekuwa namsubiri na huyu aliye mbele yangu ni mmoja,

"Bryma ndio jina lako!?", niliuliza

Alitikisa kichwa, "mbona kama umeduwaa?"

Kabla sijajibu hili swali,

"Bryma! Uko wapi? Unahitajika huku mbele tafadhari", MC aliita tena.

"duo, uugh? How about you hold that thought", alisema Bryma

Kisha aliondoka kuelekea jukwaani kwa mwendo wa madoido huku macho yangu yakimsindikiza huku nikitabasamu kwa bahati hii.

Kutoka jukwaani baada ya dakika chache, Bryma aliaanza kuimba wimbo *The Bones* wa Maren Morris.

Kwa muda wote pale ukumbini sikutaka kingine chochote zaidi ya kuwa karibu naye,

kusikia sauti yake

na kutizama sura yake.

Nikiwa bado niko chumbani nimelala nilihisi huwenda nilikuwa na mahusiano na wanawake wawili tofauti, Bryma niliyetoka kumuona kwenye simu yangu akinichafua mitandaoni na yule Bryma niliyekutana nae siku ya sherehe ya Baraka na Joan.

MWISHO

KAZI ZINGINE ZA SHAMTE KILALILE

Vitabu vya Riwaya

1. [Nyuma ya Pazia la Utawa](#)
2. [Msaliti](#)
3. [Mpango Kabambe](#)

Vitabu vya Simulizi Fupi

1. Natamani Kukusahau

Miswada ya Filamu

1. [Nyuma ya Pazia la Utawa](#)
2. [Mpango Kabambe](#)
3. [100](#) (lugha ya Kiingereza)

Vitabu vya Mahusiano & Mapenzi

1. Aina 8 Za Wanaume Zinazowavutia Wanawake
2. Aina 6 Za Wanaume Zisizowavutia Wanawake

Vitabu vya Bishara

1. Personal Guide: How to Become an Entrepreneur

KUHUSU MUANDISHI

Shamte Kilalile anaishi Dar es Salaam, Tanzania na ni mhitimu wa shahada ya Uchumi na Mipango kutoka Chuo Kikuu Mzumbe, Morogoro. Amebobeza katika Ujasiriamali, Masoko, Uandishi wa Matangazo (*Copywriting*), Uandishi wa vitabu na Uandishi wa miswada ya filamu. Na ni mwanagenzi katika fani ya *Coding*.

Ni mwanzilishi wa SparkCopy na anatoa huduma za;

1. uandishi wa riwaya (*novels*), vitabu vya biashara/ujasiriliamali au miswada ya filamu (*scripts*) kwa watu wenye stori au mawazo vichwani mwao lakini hawezi kuandika vitabu au miswada kwa ajili ya filamu wanazotaka kuzitengeneza.
2. uandishi wa matangazo ya redio, televisheni, kubrandi ukurasa wa LinkedIn, *motivation letter* au *statement of purpose* kwa wanafunzi wanaokwenda vyuo vikuu vya nje na *cv/resume*.

Kujua zaidi huduma hizi tembelea tovuti
<https://sparkcopy.wordpress.com/>

Ni mtaalamu wa masoko (*marketing consultant*) na anatoa huduma kwa wafanyabiashara wanaohitaji msaada kubusti masoko kwa ajili ya biashara zao. Kujua zaidi huduma hii tembelea tovuti:
<https://yourmarcon.wordpress.com/>

Ni dalali wa kujitegemea (*independent realtor*) wa nyumba, viwanja, mashamba, hoteli, shule na vituo vya mafuta jijini Dar es Salaam. Kama atakuwa hajihusishi na uandishi wa vitabu, utaalamu wa masoko basi atakuwa akijishughulisha na shughuli hii. Kupata huduma hii tembelea tovuti:
<https://estateowners.wordpress.com/>

**Kwa mrejesho umekionaje kitabu hiki, swali kuhusu huduma
nilizotaja au ukitaka kuoda kitabu kingine**

Piga simu: +255718515321/+255759694551

Barua pepe: rkilalile@gmail.com